REVIVAL NEWS
From Revival Ministries Australia
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

***** SEPTEMBA 2020 **** SEPTEMBA 2020 **** SEPTEMBA 2020 ****

FUNDISHO YA MUNGU

Na Geoff Terran

FUNDISHO MOJA-latimiza kusudi la Mungu la milele.

Yohana 7:16-17 Yesu akawajibu, akasema, **"Mafunzo yangu si yangu mimi, ila ni yake yeye aliyenipeleka. Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu".** Neno la Mungu tulilopewa kupitia kwa Yesu pia linaitwa hapa, 'Fundisho'. Fundisho hili lina nguvu :tunaweza kulihisi likifanya kazi katika maisha yetu na kuweza kujua linatoka kwa Mungu.

Hii ndiyo ilifanyika kwa umati wakimsikiliza Petro siku ya Pendekote. Walihisi nguvu za Mungu kuwaonyesha kwamba *"**Yesu huyo mliyemsulubisha, Mungu amemfanya kuwa Bwana na Kristo"*** **(Matendo 2:36)**. ***"Tutendeje ,ndugu zetu"*** **(Matendo 2:37)** walilia! Kisha Petro akawaambia, *"**Tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtaipokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*** **(Matendo 2:38**). Waliitikia na kubadilishwa kuwa wanafunzi wa Yesu, aliye Masiha [Mfalme wa Mungu], na kupitia maisha mapya katika Ufalme wake.

Pia tunaweza kushuhudia kwamba Roho Mtakatifu hutupa uweza wa kuishi maisha mazima mapya ya haki, Amani na furaha katika Ufalme wa Mungu, (**Warumi 14:17**). Tunakuwa kiumbe kipya katika Kristo (**2Kor.5:17**), sasa tunaweza kuwa sehemu ya kutimiza kusudi la Mungu kwa kutufanya, na kwa Uumbaji wake.

Katika **Waefeso 1:10** kusudi la Mungu la mwisho limefunuliwa: *"**Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumulisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia-Naam, katika yeye huyo**"*. Kutakuwa na "***mbingu mpya na nchi mpya ,ambayo haki yakaa ndani yake"*** **(2Petro 2:13).** Haya yote Mungu atakamilisha kupitia kwa neno ambalo tayari amesema. Andiko linaita hii 'fundisho'.

'FUNDISHO' PEKEE- neno ambalo Mungu 'ametuma', linaweza kukamilisha kusudi la Mungu katika dunia.

Kuna 'mafundisho' mengi katika ulimwengu ambayo ni ya kupinga-Kristo.
Yanaitwa:

- Mafundisho ya wanadamu (Wakolosai 2:22)
- Mafundisho ya pepo (1Timotheo 4:1)
- Mafundisho tofauti na ya kigeni (Waebrania 13:9)
- Kila upepo wa elimu (Waefeso 4:14)

- Mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo (Mathayo 16:12)

Mafundisho haya yote hayaelekezi kwa uzima bali hakika kwa mauti. "**Mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo"(Mathayo 7:13).**

Kuna MOJA pekee, 'Fundisho la Mungu'

1. Yesu Kristo ndiye Fundisho [Neno la Mungu] lililofanyika mwili.

Mara baada ya kufufuka kwake, Yesu alitembea na wanafunzi wawili wakirudi Emau ambao waliogopa alikuwa amekufa. Aliwaambia, ***"Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini waliyoyasema manabii. Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?*** **(Luka 24:25).** ***Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaelezea katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe"*** **(Luka 24:27)**. Maandiko yote yanaelekeza kwa Yesu na yametimia ndani yake. Yesu ni Neno lililofanywa kuwa mwili. Aliamini na kufundisha kutoka 'Maandiko yote '.

Katika **Yohana 1:14**, tunasoma kwamba *"**Naye Neno likafanyika kuwa mwili, akakaa kwetu, nasi tukaliona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa baba, amejaa neema na kweli"***. Yesu kama 'Mwana wa pekee' alifunua kikamilifu na **'kutangaza'** yule Mungu ni, na jinsi Mungu alivyo. (**Yn.1:18**).

"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake" **Waebrania 1:1-3**. Katika Uumbaji, Yesu ndiye Yule ambaye kupitia kwake Mungu **aliunena** ulimwengu kuwa, na bado anaushikilia wote kwa **Neno la uweza wake'** [Angalia Mwanzo 1-Mungu anaunena ulimwengu kuwa].

Kama Mtume wetu, (Waebrania 3:1) Yesu alimtambulisha Mungu kwa mwanadamu. Alituonyesha jinsi Mungu alivyo. Sehemu muhimu ya kazi yake ilikuwa ni kuwatayarisha mitume kumi na wawili ambao wangeendeleza huduma yake na kujenga kanisa lake kwa kunena fundisho la kweli pekee.

2. Yale yote ambayo Yesu alifundisha ndiyo 'Fundisho'.

"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe" **(Mathayo 24:35).** Maneno ya Yesu ni Kweli ya milele! Na tayari tumeona ya kwamba Yesu aliamini 'Maandiko yote' na akafundisha kutoka kwayo.

Luka 4:17-19 ni mfano wa nguvu wa jinsi Yesu alitumia neno la Mungu kwa maisha yake na huduma. ***"Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo akatafuta mahali palipoandikwa, <u>Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa; Na kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa</u>" Kisha Yesu akatangaza: 'Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu'. Maisha yake yalitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale kuhusu Masiha.***

Kisha Yesu akaanza huduma yake hadharani kuhubiri Injili ya Ufalme wa Mungu, akisema: ***"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni, na kuamini Injili"*** **Mariko 1:15.**

Yesu alifundisha kwa mamlaka

"Wakashangaa mno kwa mafundisho yake, kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri ,wala si kama waandishi" **Mariko 1:22**.Wakashangaa wote, hata wakaulizana, wakisema, ***"Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wamtii!"*** **(mst.27**).

Fundisho la Mungu

Wayahudi waliposhangaa jinsi Yesu alifundisha katika Hekalu, Aliwajibu: ***"Mafunzo yangu si yangu mimi, ila ni yake yeye aliyenipeleka. Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya***

yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yang tu. Yeye anenaye kwa nafsi yake tu hutafuta utukufu wake mwenyewe; bali yeye anayetafuta utukufu wake aliyempeleka huyo ni wa kweli, wala ndani yake hamna udhalimu" **Yohana 7:16-18**.

Ni yule tu 'aliyetumwa' anayeweza kufanya hii, kutafuta utukufu wa Mungu pekee, Mtumaji. Mafunzo ambayo Yesu alipokea kutoka kwa Baba yake yalitolewa kupitia kwake kama Mwana. Alikuwa Moja na Baba, hakuwa na ajenda ya kibinafsi.

3. Kama vile Yesu ALIVYOTUMWA na Baba kunena maneno yake, mitume WAMETUMWA na Yesu.

- Wakati wa huduma yake ya miaka -mitatu, Yesu alifundisha kwa mfano; kisha akawatuma wanafunzi nje kufanya vile alivyofanya, na kurudisha ripoti (**Mathayo 10:40**).
- Kabla tu ya kwenda msalabani Yesu aliomba **"Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao, nao wakayapokea ,wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasidiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma"(Yohana 17:8).**
- Katika **Mathayo 28:18-20** baada ya kufufuka kwake ,Yesu aliwatuma Mitume wake –kama vile tu alivyotumwa na Baba yake. Yesu alikuja na kunena nao, akisema***, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru; na tazama mimi nipo nanyi siku zote, hata ukamilifu wa Dahari. Amina".***

4. Mafunzo ya Yesu yanakuwa Mafunzo ya Mitume.

"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika na katika kuumega mkate, na katika kusali" Matendo 2:42. Hizo ndizo zilikuwa kazi za kwanza za kanisa la kwanza ambazo zilileta matokeo ya ajabu: fundisho la mitume, ushirika, kuumega mkate na kusali.

Katika **Warumi 6:17,18** mtume Paulo anaandika: ***"Lakini Mungu ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile <u>namna ya elimu</u> ambayo mliwekwa chini yake, na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi".*** Ingawa Paulo hakuwa mmoja ya wale mitume kumi na wawili ambao Yesu aliwafundisha, fundisho lake lilitoka kwa Yesu (**1Kor.3:15a;1Kor.11:23a**). 'Fundisho la Mitume' lina uweza wa kufunua Yesu na kubadilisha maisha.

Katika **1Timotheo 6** Paulo anafundisha bwana na watumwa kuhusiana katika upendo kama ndugu katika Kristo, kisha anasema katika msitari **3-4:** ***"Mtu awaye yote akifundisha elimu nyingine, wala hayakubali maneno yenye uzima ya Bwana wetu Yesu Kristo, wala mafundisho yapatanayo na utauwa, amejivuna ;wala hafahamu neno lo lote".***Na mwishowe, ***"…wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida. Jitenge na watu kama hawa"*** **(mst.5).**

5. Fundisho la Mitume linajumuisha Andiko yote!

"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza , na kwa kuwaadibisha katika haki" **2Timitheo 3:16.**

Nimeshawishika tena, kwamba ni muhimu **kuamini kile ninasoma katika Maandiko**, na **si tu kusoma kile ambacho tayari naamini**. Tazama kwa makini tofauti.

Katika **Tito 2:7** Paulo anahimiza ***" Katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu"***.Tunafaa kushika neno la Mungu kwa usahihi, heshima na ustahivu. Sema neno tu: bila kuongezea kwa yaliyoandikwa- bila kutoa kwayo! Hii ni ngumu kama kuna pingamizi za uaminifu kwa mafundisho ya kidini.

***"Maana utakuja wakati watakapokataa mafundisho yenye uzima ;ila kwa kuzitafuta nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti"* 2Timotheo 4:3**. Hawa wanafuata walimu ambao wanasema yale wanataka kusikia: kuhusu mali, starehe za kidunia, ufanisi na kadhalika. Fundisho la ufanisi, na ' kukwepa kwa kunyakuliwa' ni mifano ya hii. Wamechanganya wengi, kuwaelekeza mbali na kuelewa kusudi la Mungu na kulifuata.

"*Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu .Yeye adumuye katika mafundisho hayo ,huyo ana Baba na Mwana pia."* 2Yohana1:9.

'Fundisho la Kristo' ni ufunuo wa kwanza wa yule Yesu ni. Maandiko yote yanafunua Yesu na yanafundisha wazi ya kuwa jina 'Yesu' linamaanisha 'Mungu kutuokoa' (**Mathayo 1:21**). 'Kristo' ni kigiriki kwa 'Masiha' ya kihibrania, ambalo linamaanisha 'Mfalme wa Mungu aliyepakwa mafuta'-na Yesu ni Mfalme sasa (Matendo 2:36).Tunapobaki, au 'kudumu' katika ufunuo huu tunakua kujua na kumpenda Yesu –na anamfunua Baba kwetu kama wana wake.

6. Fundisho la Mitume ,linapofundishwa kupitia kwa vipawa-vitano vya Yesu, kwa Bi harusi yake Kanisa- humleta kwa 'imani moja' na kwa 'kimo cha ukamilifu cha Kristo'.

Katika kupaa kwake, Yesu alitoa kipawa cha sehemu tano kwa kanisa lake kumleta kwa umoja katika Kristo. Kuna 'imani moja', ambayo huja kutokana kufundisha 'fundisho la Mungu':fundisho la mitume.(**Waefeso 4:4-7**).

***"Naye alitoa wengine kuwa mitume ,na wengine kuwa manabii,na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"* (Waefeso 4:11-13).**

> Neno la Kigiriki kwa 'ku' hutafsiriwa 'kwenye' -ambalo linaingia vizuri hapa. Dini hutufinyilia kuwa kitu ambacho hatuko. Fundisho la Mitume hutuita 'kwenye' Yule ambaye ni 4aisha yetu- na ambaye ni mkamilifu.

Yesu alikuwa sadaka ya dhambi kwetu ili tuweze kupokea haki yake (2Kor.5:21). Mungu hutuona 'katika Kristo' na kutupa haki ya Yesu -tungali bado katika njia ya kubadilishwa **"kwenye mfano sawa"(**2Kor.3:18).Yeye hutuona wewe na mimi, 'kufanywa haki'-kama tu sikuwahi kutenda dhambi -kama bado tuko njiani kuja ***"kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"* (Waefeso 4:13b**}pamoja. Hakuna hata moja ya hizi ni kwa nguvu zetu wenyewe bali kupitia kwa imani kwa Mungu, na neno lake la kweli-'fundisho'-ambalo huleta neema ya kuwezesha.

Katika **Waefeso 5**, tunapata kwamba Yesu anamwosha Bi harusi yake ***"kwa kulisafisha kwa maji katika neno ,apate kujiletea kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo"* (mst.26-27).**

Katika sura **ya 4** tunaona huduma ya Yesu ya neema ilikuwa kupitia **kipawa** chake (**mst.7**), ambacho ni mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu (**mst.11**). Pamoja vipawa hivi vinaleta kanisa lake kwa '**umoja wa imani'** na '**kwenye** mtu mtimilifu' (**Waefeso 4:13**).

***"Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana , kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho ,na kuamini kweli; aliyowaitia ninyi kwa injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo"* 2Thes.2:13-14).**

7. **‘Fundisho la Mungu linafaa kujaza kila mahali- na mwishowe,ku ‘kusanya pamoja kwa MOJA, vitu vyote katika Kristo’.**

“Je! Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa jina hili? Nanyi ,tazameni mmeijaza Yerusalemu fundisho yenu” Matendo 5:28*. Fundisho la Mungu ni kuhubiri na kufundisha Yesu aliye Kristo!* ***“Na kila siku ,ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo”*** **Matendo 5:42**. Ni fundisho gani unanena? Je, fundisho lako linamfahamisha Yesu aliye Kristo?

Habakuki 2:14 Mungu kila mara amekusudia dunia yote kujazwa maarifa ya utukufu wa Bwana. Hii inaweza kufanyika aje? Kwa kufundisha na kuhubiri fundisho hili!

Mungu atatimiza neno lake:

- Bi harusi mwenye utukufu atatokea na kukutana na Bwana harusi yake (**Waefeso4:13&5:27**)
- Wana wanaoendelea katika imani wataona kufanyika kwao kuwa wana ukikamilishwa na mwili wa ufufuo! (**Warumi 8:23**}
- Uumbaji wenyewe utawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu’ hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu’ (**Warumi 8:21**)
- “Mbingu mpya na nchi mpya ambayo haki yakaa ndani yake” itakuwa hakika (**2Petro 3:13**)
- Kuleta pamoja vitu vyote ‘ndani ya Kristo’ itakamilishwa (**Waefeso 1:10**).

Katika **Matendo 1:1**, Luka mwandishi, anasema kuhusu ‘kile kitabu cha kwanza alichokiandika’[Injili ya Luka], kwamba ilikuwa juu ya vitu ambavyo Yesu alianza kufanya na kufundisha. Kisha katika Matendo anatoa rikodi ya huduma inayoendelea ya Yesu kupitia kwa wanafunzi wake. Wao pia wanakuwa ‘barua zilizohai’ za ‘fundisho’, kufanya Yesu kuonekana, na kuleta mbinguni duniani.

Sasa ni zamu yetu. Kama watu wa kitume, tume‘tumwa’ kuwa sehemu ya huduma ya Yesu inayoendelea katika kizazi chetu. Ametuita kila mmoja kwa jina kwa wakati kama huu! Amina.

Yesu Kristo ndiye
‘fundisho’ na Maandiko yote
yanaelekeza kwake.
Ni ‘fundisho’ pekee
lililotolewa na Mungu
kupitia Yesu kwa Mitume wake
lina uwezo na mamlaka kutimiza
kusudi lake la milele
na ‘kuleta pamoja kwa MOJA
vitu vyote
KATIKA KRISTO’.